HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

SHULE YA SEKONDARI MWAYA,

S.L.P 130,

KYELA.

04.12.2020

MOB. 0764974299

Kumb na. MOESTV/S2293

Jina la mwanafunzi ……

S. L. P ……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWAYA WILAYA YA KYELA MKOA WA MBEYA MWAKA 2021.

1.0: Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Mwaya iliyopo na umbali wa kilomita 9.2 kutoka ofisi ya halmashauri ya Kyela. Usafiri wa basi unapatikana katika kituo cha mabasi ya stendi kuu ambapo nauli ni Tsh. 1,000/= kufika shuleni kwa kutumia gari.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti kuanzia tarehe 04/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 15/01/2021 ndani ya siku saba.

2.0: **Mambo muhimu ya kuzingatia**

2.1: Sare za shule

a) i) **Wavulana –** suruali moja ya kijani na moja nyeusi, soksi nyeusi, na mashati mawili meupe ya mikono mifupi. Suruali ya kijani ya kuiva na nyeusi zenye malinda na mfuko mmoja nyuma, Suruali nyembamba (modal) haitakiwi hivyo taratibu zitafuatwa kwa mwanafunzi atakae kiuka agizo hilo. Pia mkanda wa suruali uwe mweusi na usiwe na chuma kikubwa.

ii) **wasichana** – sketi moja ya kijani na moja nyeusi, soksi nyeupe na mashati meupe mawili mikono mifupi. Sketi ya kijani ya kuiva na nyeusi zenye malinda madogo ya kawaida. Pia sketi ziwe ndefu sana zakugusa soksi.

b) Rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule hasa nyeupe

c) Sare za michezo

i) **Wavulana.** Viatu vya michezo, bukta ya bluu na fulana ya blue moja

ii) **Wasichana-** Viatu vya michezo (Raba nyeupe) Track suit ya blue na fulana ya blue

d) Kila mwanafunzi aje na T- shirt ya rangi ugoro yenye kola yenye ufito wa bendera ya Taifa ambayo pia itapatikana shuleni kwa utaratibu utakao andaliwa (Gharama ya Tshs. 10,000/=) pia wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na sweta la blue hasa wakatika wa baridi.

e) Begi la shule la mgongoni.

f) Viatu vya shule vya ngozi vyeusi vyenye kamba na kisigino kifupi

2.2 Mwanafunzi anatakiwa kuwa na daftari zisizopungua (9) (counter book 2 quire) kalamu na mkebe wa hesabu pamoja na kamusi ya kiingereza.

2.3: Mzazi kugharamia chakula cha wanafunzi ya kutwa,nauli ya kwenda na kurudi pamoja na matibabu

2.3: Mwanafunzi pia anatakiwa kuja na Tsh. 20,000/= ya chakula na bunda (rim) moja ya karatasi za A_4 kwaajili ya majaribio mbalimbali yatakayo tolewa na walimu. Haya ni makubaliano ya kamati ya wazazi

NB: Zingatia maagizo hayo kwani yatazingatiwa wakati wa kuripoti mwanafunzi

3.0: Sheria na kanuni muhimu za shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria na. 10 ya mwaka 1995 aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya elimu yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Raisi TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d. Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa wanafunzi wawapo katika shule hii.
f. Kutunza usafi wa mwili, Mavazi na mazingira ya shule
g. Kuva sare ya shule wakati wote unao takiwa
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
i. Kutunza mali za umma

3.1 **Makosa yanayoweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.**

a. Wizi
b. Uasherati na Ushoga
c. Ubakaji
d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji Bangi, Cocaine, Mirungi, Kuberi na mengineyo.
e. Kupigana au kupiga
f. Kuharibu kwa makusudi mali za umma
g. Kudharau bendera ya Taifa
h. Kuwa mjamzito/ kupata mimba
i. Kuoa au kuolewa
j. Kutoa mimba
k. Kugoma, Kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
l. Kukataa adhabu kwa makusudi

m. Kuwa na simu ya mkononi

PRESIDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

KYELA DISTRICT COUNCIL

MWAYASECONDARY SCHOOL. P O BOX 130 KYELA - MBEYA

DATE ……....

REF. NO, MOESTV/ S2293

The medical officer

……..

PART A:

RE: EXAMINATION OF MR/MISS ……..

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time student in this school. The examination should include the following categories

1. Hemoglobin _____
2. P.V. Bleeding_____
3. Sight _____
4. Blood pressure _____
5. Urine for sugar and pregnancy test _____
6. Stool for routine examination _____
7. Asthma _____
8. Skin diseases _____
9. Leprosy _____
10. Any deformity _____
11. Epilepsy _____
12. Pulmonary tuberculosis _____
13. Neurosis _____
14. Venereal diseases _____
15. Other serious diseases _____

PART B:

(To be completed by Government medical Officer)

I have examine the above named and consider that he/she physical and mental fit/unfit for full schooling